

## Mazao

Nyasi ya kufunikia - tani 4.63 kwa kila hekta

Karatasi ya nailoni - tani 5.2 kwa kila hekta

Kupalilia kila wiki 2 - tani 4.69 kwa kila hekta

Kutumia nyasi ni bora zaidi kuliko kupalilia kwa sababu gharama ni ya chini mno.



Kutumia karatasi ya nailoni kunapunguza gharama



Vitunguu vya kiwango cha juu



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www. kari.org

#### Mtayarishaji:

Waiganjo. M

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Thika,

S.L.P.1220- thika

Simu: 067 21281/5, 21134 au 2055038

Nukulishi: 067 21285

Baruapepe: karithika@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 36 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Dhibiti kwekwe kwenye vitunguu-viazi ili kuongeza mazao



## Utangulizi

Vitunguu viazi ni nambari ya tatu katika umuhimu katika masoko ya humu nchini. Hukua vizuri katika viwango vya mita 1,900 juu ya bahari na mvua ya milimita 500-700 na kiasi cha joto cha nyuzi 15-30; mchanga wenye rutuba usiokuwa na maji mengi na kiwango cha maji (pH) cha katia ya 5.8-6.5.

Mmea wa kitunguu una mizizi miembamba ya juu inayotoka kwenye mihimili inayosababisha ushindani mkali sana na mimea mingine yenye mizizi mipana.

Iwapo kuna makwekwe mengi, mimea ya vitunguu huonyesha dalili za unyonge na wakati mwingine kusababisha kufeli kwa mazao.

Namana mbali mbali za udhibiti wa kwekwe hutumiwa pamoja na kulimia, madawa na kuyafunikia magugu.

## Kulimia kwa mikono

Kutumia wafanya kazi wengi. Mtindo wa kulima kwa mikono umeendelea na wakulima wengi humu nchini Kenya. Mtindo huu huchosha na huhitaji wafanyakazi wengi.

## Madawa

Matumizi ya madawa kabla ya kwekwe kutokeza unaofanywa wiki mbili baada ya kupandwa hudhibiti vitungu katika kipindi chote cha kukua.



Shamba lilolimwa kwa mikono

## Mbolea za nyumbani na za dukani za kufunikia

### i) Kifunkio cha nyasi

Mchanga katika eneo la mihimili ya vitunguu hufunikwa kwa sentimita 5 kwa nyasi iliyokauka wiki 2 baada ya kupandwa na kuachwa hivyo hadi mwisho wa msimu.



Kifunikio kikavu

Mashambulizi ya mchwa yanaweza kupelekea haja ya kuongezea nyasi baada ya mwaka mmoja.

### ii) Kifuniko cha karatasi nyeusi ya nailoni

Karatasi nyeusi ya nailoni hutandazwa chini juu ya mchanga kabla ya kupanda vitunguu. Mashino ya kupanda yanatobolewa kwenye karatasi hiyo kwa umbali wa sentimita 10x20. Hii hufanywa katika shamba lote na husalia hapo hadi mwisho wa msimu.



Karatasi nyeusi ya kufunikia

Mimea ya vitunguu iliyopandwa kwenye vifunikio vya nyasi au karatasi hiyo ya plastiki haihitaji kupaliliwa. Hii ni kwa sababu kwekwe pamoja na unyevu huzuiliwa na vifunikio hivyo na vitunguu hivyo hutoa mazao bora na kiwango cha juu zaidi.